# HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

SHULE YA SEKONDARI YALAWE

S.L.P 3783, MBEYA

20/12/2020

KUMB.NA YASS/S.3744/ADM/VOL2/........

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI...........................................................................................

YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YALAWE

Ninayofuraha kukupongeza na kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Yalawe mwaka 2020. Shule ya sekondari Yalawe ni ya kutwa na ni ya mchanganyiko yaani wavulana na wasichana. Shule ipo katika kata ya Santilya.
Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11.01.2021 saa 1:30 asubuhi bila kukosa. Kuchelewa kuripoti kwa muda muafaka anaweza kupoteza nafasi yake.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A. SARE ZA SHULE

| Na | Wavulana | Wasichana |
|---|---|---|
| 1. | Suruali mbili(2) nyeusi na kijani zenye turnup na marinda na zisiwe modal | Sketi mbili(2) nyeusi na kijani zenye marinda na urefu wa sketi upite magoti |
| 2. | Shati mbili(2) nyeupe za tetroni za mikono mifupi | Shati mbili(2) nyeupe za tetroni za mikono mifupi |
| 3. | Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi vya kamba na visiwe na visigino virefu | Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi vya kamba na visiwe na visigino virefu |
| 4. | Masweta mawili(2) ya kijani kwa ajili ya kujikinga na baridi | Masweta mawili(2) ya kijani kwa ajili ya kujikinga na baridi |
| 5. | Mkanda mweusi wa suruali wa ngozi | Jozi mbili(2) za soksi nyeupe |
| 6. | Jozi mbili(2) za soksi nyeusi | Nguo za michezo raba nyeusi, trucksut nyeusi, gauni jeupe mshono wa solo na litashonwa kwa maelekezo ya mwalimu wa michezo shuleni |
| 7. | Nguo za michezo trucksut nyeusi, t shirt nyeupe na raba nyeusi | |

B. MAAGIZO MENGINE

1. Madaftari (Caunter book Q3) kumi na mbili(12) na kalamu za kutosha
2. Beg la kubebea madaftari
3. Mkebe(Mathematical set)
4. Flat file kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake
5. Nakala ya cheti cha kuzaliwa

C. VIFAA VYA USAFI

1. Jembe lenye mpini kwa wavulana
2. Mfagio wa chelewa na ndoo ya lita kumi kwa wasichana

***MUHIMU***

Pamoja na maagizo haya nimeambatanisha

1. Sheria na kanuni za shule
2. Fomu ya afya(mpeleke mwanao hospitali kuchunguza afya yake kabla ya kumleta shuleni)

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia yote inayoletewa na na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

1. Wanafunzi wanahitajika kuishi kwa amani na upendo hapa shuleni. Ugonvi wa aina yoyote ile ni marufuku, kauli zako muda wote zionyeshe busara na upendo. Kuandika matusi kwenye kuta au mbao za darasani au popote ni uharibifu na ni marufuku.
2. Mali ya shule pamoja na yako binafsi ni lazima itunzwe vyema. Kufanya kitendo chochote ambacho kinaweza kuharibu mali ya shule au yako ni kosa kubwa. Kutokana na uzito wa kosa unaweza kufukuzwa shule.
3. Nidhamu inahitajika darasani na nje ya darasa. Huruhusiwi kupiga kelele darasani au kutoka darasani bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa. Mtindo wa kuzomeana ni marufuku hapa shuleni kwani sio uungwana. Mwanafunzi anapoulizwa swali ni lazima anyoshe mkono wa kulia na asimame kuijibu.
4. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kusimama kwa adabu anapoingia mwalimu au kiongozi yeyote anapofika darasani au shuleni kwa ujumla.
5. Ni lazima mwanafunzi aheshimu ofisi ya Mkuu wa shule.Walimu na makarani, hakuna ruhusa kuingia ofisini na nyumba za walimu na wafanyakazi bila idhini ya mkuu wa shule
6. Ni lazima mwanafunzi aheshimu bendera ya Taifa na picha za viongozi wa Taifa letu, kinyume hicho mwanafunzi huyo atachukuliwa hatua kali.
7. Mwanafunzi anapozungumza na mwalimu au mkubwa wake yeyote asiweke mkono mfukoni au kushika kiuno na kubishana kwa dharau pia mwanafunzi anapoitwa na mwalimu au mkubwa yeyote ni lazima akimbie haraka.
8. Mwanafunzi akishaingia katika eneo la shule haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule hadi anaporudi nyumbani au kwa kibali maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu
9. Unatakiwa kuhudhuria shughuli zote za shule za ndani na nje ya darasa
10. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule, kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
11. Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote

## KUFUKUZWA SHULE

Yafuatayo ni makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule

i. Wizi
ii. Uasherati, ubakaji au ushoga
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
iv. Makosa ya jinai
v. Uvutaji bangi
vi. Kupigana au kupiga
vii. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
viii. Kudharau bendera ya Taifa
ix. Kuoa au kuolewa
x. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule
xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
xii. Kukataa adhabu kwa makusudi

NB: Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu shuleni, akikamatwa na simu ataiharibu mwenyewe na atapewa adhabu kali.

Mambo mengine muhimu yanapaswa kukamilishwa na kuwasilishwa na mwanafunzi pamoja na fomu ya maelekezo kutoka kwa daktari juu ya afya ya mwanafunzi.

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana Yalawe Sekondari.

***"Education for Liberation"***

......................

**DAUDI A. KITIKU**
**MKUU WA SHULE**

MINISTRY OF EDUCATION,SCIENCE AND VOCATIONAL TRAINING

YALAWE SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 3783
MBEYA
Date.........................

THE MEDICAL OFFICER
...................................................
...................................................
...................................................

**PART "A"**
Mr/Mss...............................................................Please examine the student(name)..........................................................................his/her physical and mental fitness for a full time student in the school. The exmination should include the following

1. Haemoglobin ...........................................................................
2. P.V Bleeding...........................................................................
3. Sight.......................................................................................
4. Blood pressure.........................................................................
5. Urine for sugar and pregnancy test........................................
6. Stool for routine examination.................................................
7. Asthma...................................................................................
8. Skin diseases..........................................................................
9. Leprosy..................................................................................
10. Any deformity......................................................................
11. Epilepsy ..................................................................................
12. Pulmonary tuberclosis............................................................
13. Neurosis..................................................................................
14. Veneral diseases.........................................................................
15. Other serious diseases...............................................................

**PART "B" MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by an gorvernment medical officer)

I have examined the above student and I recommend that he/she is fit/not fit for full time schooling...........................................................................................................................
Other comments...............................................................................................................

Date .......................

Signature ........................................
stamp